OFISI YA RAIS-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA ULANGA

SHULE YA SEKONDARI MAHENGE,
S.L.P 14,
MAHENGE /ULANGA
TAREHE………………

Kwa mzazi/mlezi wa ……………………………………………………………………

YAH: <u>MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE</u>

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari Mahenge kidato cha Kwanza kwa mwaka wa masomo wa ………………………..

Aidha uongozi wa shule unachukua fursa hii kukupongeza na kukukaribisha Mahenge Sekondari.

Mahenge Sekondari ni shule ya sekondari ya serikali ya kutwa kwa Wasichana na Wavulana, ipo umbali wa 0.5 km (Nusu kilomita) kutoka yalipo makao makuu ya Wilaya, Kasikazini mwa mji wa Mahenge. Shule itafunguliwa rasmi kwa muhula wa kwanza tarehe ………….. Aidha utatakiwa kujibidisha katika masomo yako kwa muda wote utakaokuwepo hapa shuleni kama mwanafunzi na kwamba uzembe na uvivu wa kujisomea kwa bidii utapelekea kushindwa kuendelea na masomo yako kwani ufaulu wako pia utakuwa hafifu.

SARE ZA SHULE

(A)WAVULANA

(i) SURUALI: Rangi ya kitambaa ni **bluu nyeusi** (Dark blue) iliyoshonwa katika maadili yanayokubalika na jamii, isiwe ya kubana na lazima iwe na marinda mawili. Mashono yake yasiwe mfano wa jeans. Kinyume na hapo suruali hiyo haitakubalika na utalazimika kushona nyingine.

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MAHENGE
S. L. P. 14
MAHENGE /ULANGA

Scanned with CamScanner

Scanned with CamScanner

(ii) SHATI: Shati la kitambaa cheupe mikono mifupi lisilobana mwili na liwe refu kiasi cha kutosha kuchomekea kwenye suruali. Shati hilo lazima liwe na kora.

(iii) VIATU: Viwe vyeusi vya ngozi na pia vya kufunga na kamba. Visiwe na kisigino kirefu.

(iv) SOKSI: Ziwe ndefu na za rangi nyeupe.

(B) WASICHANA:

(i) SKETI : Kitambaa chake ni cha rangi ya **kijani nzito** (Dark green). Mashono yake ni ya rinda box. Sketi zishonwe ndefu hadi chini ya magoti inchi tatu, sketi ndefu zaidi ya hapo zingependeza. Sketi fupi na zisizo za kitambaa sahihi hazitavumiliwa na utalazimika kushona sketi nyingine.

(ii) BLAUZI/SHATI: Rangi ni nyeupe isiyobana mwili. Ndani ya shati msichana atavaa nguo nyingine nyeupe (shumizi) kwa lengo la kusitili mwili wake.

NB: Kwa wanafunzi wa kiisilamu watakaohitaji kuvaa hijabu, watavaa hijabu za rangi nyeupe na ziwe ndefu kuweza kufunika hadi maeneo ya mabega yao. Hijabu zote ziwe kama kitambaa cha shati la shule na zisiwe na urembo wa aina yoyote ile.

(iii) VIATU: Rangi ni nyeusi vya kufunga kwa kamba na viwe na visigino vifupi. Viatu vya wazi (open shoes) yeboyebo na bajaji haviruhusiwi.

(iv) SOKSI: Rangi ni nyeupe zisiwe na alama wala maandishi ya aina yoyote ile.

SARE ZA MICHEZO NA NGUO ZA KAZI ZA NJE

(i) Kwa wanafunzi wa kike na wakiume sare hizo ni T-shirt nyekundu yenye shingo duara kwa ajili ya shughuli za kazi za nje za mikono, pia watatakiwa kuvaa ama sketi ya shule au suruali pamoja na hiyo T-shirt wakati wa kazi hizo.

(ii) Wakati wa michezo mwanafunzi atatakiwa kuwa sketi nyeusi kwa wasichana na bukta ya bluu kwa wavulana pamoja na T-shirt zao nyekundu. Pià wakati wa michezo mwanafunzi utatakiwa kuwa na viatu vya raba.

NB: T-shirt hazitakiwi kuwa na maandishi ya aina yoyote ile. Wakati wa michezo mwanafunzi atapaswa kuvaa soksi maalumu za michezo.

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MAHENGE
S. L. P. 14
MAHENGE ULANGA

Scanned with CamScanner

Scanned with CamScanner

VIFAA VYA DARASANI:

(i) Madaftari 11 (kumi na moja) counter book quire 2 au 3 kwa ajili ya masomo kumi na moja atakayofundishwa hapa shuleni.

(ii) Mkebe wa hisabati (mathematical set)

(iii) Peni iwe bluu au nyeusi

(iv) Rula, penseli, kifutio n.k

NB: Kutokana na uahaba wa vitabu uliopo shuleni kwa masomo ya sanaa na lugha unashauriwa kununua vitabu kwa ajili yako ili kuongeza ufanisi katika kujisomea kwako. Masomo hayo ni Historia, Jiografia, Uraia, Kiingereza na Kiswahili.

Utakapofika shuleni utapewa na kuelekezwa sheria za shule ambazo kipindi chote utakapokuwa shuleni utatakiwa kuzifuata, kuzitii na kuziheshimu, kinyume na hapo utapewa adhabu kali ikiwa pamoja na kufukuzwa shule.

Nakukaribisha sana Mahenge Sekondari shule yenye mandhari nzuri ya kusoma

....

Mkuu wa Shule

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MAHENGE
S. L. P. 14
MAHENGE ULANGA

Scanned with CamScanner

Scanned with CamScanner

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATION TANZANIA
STUDENT MEDICAL CERTIFICATE.

To be completed by a Government Medical Officer and returned to the Headmaster of MAHENGE SECONDARY SCHOOL, P.O.BOX 14, MAHENGE/ULANGA.

Date.......................................

To the Medical Officer

....

REF: ____

Please , examine the above named student and comment on his/her health status by responding to the following items. Kindly put a tick (√) or a cross (x) in front of either Yes or No.

HEADMASTER.

Does the student has problems in connection with

(a) Sight?...YES/NO

If Yes, state...

(b) Hearing ?...YES/NO

If Yes, state...

(c) Speech? ....YES/NO

If Yes, state...

(d) T.B?...YES/NO

If Yes, state...

(e) Blood

pressure?..YES/NO

If Yes, state...

(f) Any physical disability?...YES/NO

If Yes, state...

Do you recommended him/her that she/he is physically fit for studies at school? YES/NO? If NO, Please state the reasons...

FOMU HII IRUDISHWE SHULENI KWA MKUU WA SHULE KABLA AU SIKU YA KUFUNGUA SHULE

Scanned with CamScanner

Scanned with CamScanner